


Mashairi ya Amanda

Kusherehe
kea Maisha ya
Amanda na
Kushiriki
Ujumbe Wake
Kupitia
Mashairi
Yake

Mashairi ya Kutia Moyo–
yanayotia nguvu, matumaini, na imani
wakati wa dhiki

Ishi kwa imani, si kwa kuona.

2 Wakorintho 5:7



Mashairi kwenye kurasa zifuatazo ni dhihirisho la hisia mbalimbali za Amanda. Maneno yake yanaeleza jinsi uhusiano wake na Mungu ulivyomsaidia katika nyakati ngumu na kuwa mwenye shukrani, hata upitiapo matatizo makubwa. Tamanio la Amanda lilikuwa kuwa mashairi yake yachapishwe na kupewa wengine ili yawatie moyo na kuonyesha jinsi alivyopata nguvu kutokana na imani yake – huu ni ujumbe wa Amanda.

Yaliyomo

1 KUSHEREHEKEA MAISHA YA AMANDA

5 MAMBO MADOGO
Amanda alijifunza kuthamini mambo madogo maishani.

7 KUVUNJIKA MOYO KUNA BARAKA
Katika majaribu Amanda alihisi uwepo wa Mungu na imani yake ikaimarika zaidi.

8 BARAKA ZISIZO TARAJIWA
Amanda alijua kwamba maisha yake hayangesalia jinsi yalivyokuwa, kwani aliachana na mambo yaliyopita na kukumbatia yajayo ambayo Mungu alimpangia huku akielekeza macho yake kwa Bwana

9 SIKU BORA ZAIDI
Wakati wa matibabu yake aliandika, "... hadi wakati ambapo mawazo ya siku bora sio mawazo tu."

11 SI JIBU NILILOTARAJIA
Amanda aliandika shairi hili baada ya vipimo kuonyesha saratani imerejea.

12 KUVUMILIA KATIKA MAOMBI
Katika shairi hili Amanda anajisalimisha kikamilifu kwa mpango wa Mungu kwa ajili ya maisha yake.

13 SHUGHULI NYINGI MAISHANI
Amanda hakuruhusu wasiwasi kumtawala kwani aliomba kila siku.

14 AHADI ZILIZOTIMIZWA
Madaktari walihofia kuwa huenda saratani ya Amanda ilirejea; hata hivyo, Aaron Dieppa alikuwa amempenda Amanda na aliazimia kumuoa. Katika sherehe nzuri ya harusi mnamo 15/11/03 aliolewa na akawa Amanda Dieppa.

15 NIMEPOTEZA VYOTE
Baada ya miezi 3 ya ndoa, Amanda akafadhaishwa na habari kwamba saratani yake imerejea. Kutokana na imani yake katika Bwana na uwepo wa Aaron , alisimama imara.

16 KIKOMBE KILICHOJAA POMONI Miaka ya kupambana na saratani ilikuwa ikimwathiri Amanda. Yeye ni mnyonge na dhaifu; lakini anaamini, kumtumainia na kumngoja Mungu ili siku moja ajaze kikombe chake hadi kifurike.

17 KUWA NA MUNGU MOYONI

Katika shairi hili Amanda anaelezea umuhimu wa kuwa na Kristo moyoni. Alihoji kwa nini watu wanajaribu kuweka kila kitu isipokuwa Mungu ndani ya nafasi ya moyo wao alioutengeneza Mungu.

18 KUENDELEA KUJISALIMISHA

Mungu anampa muda Amanda Amanda anapojisalimisha kwa mpango Wake kwa maisha yake.

19 WAKATI WA KUKATA TAMAA

Baada ya miaka sita ya kupambana na saratani, Amanda anahisi kutokuwa na tumaini na mwenye huzuni nyingi; lakini anafarijiwa na tumaini la milele la Mungu na ahadi ya maisha ya baadaye.

20 BAADA YA MUDA MFUPI

Amanda anahisi mwenye shukrani, anayependwa, aliyejazwa na mwenye amani na anamngojea Bwana kutimiza ahadi Yake...tayari baada ya muda mfupi.

21 YAFUNGUE MACHO YANGU

Amanda anaomba Mungu amfungue macho ya kiroho ili aone mpango Wake kwa maisha yake.

23 UTELE

Amanda anaandika kuhusu hali ya utulivu uletwao na ukamilifu kwani anaanza kuona kusudi la Mungu kwa maisha yake na anajitahidi kuishi kulingana na mpango Wake.

24 MAJARIBU YA MUDA

Imani ya Amanda inaendelea kukua kama Mungu anapomsaidia katika dhoruba za maisha.

25 MATUMAINI YASIYO NA MWISHO

Amanda anaahidi kumtukuza Mungu hadi mwisho, hata katika mauti, anaposonga mbele akijua kwamba, chaguo za kupata tiba zinazidi kuwa finyu.

26 NINA MZIGO WA MILELE

Hii ni siku ya huzuni kwa Amanda na anaandika shairi hili baada ya vipimo kudhihirisha kuwa saratani yake bado inazidi kuongezeka.

27 OKOTA VIPANDE

Maisha ya Amanda yalivurugwa na habari siku tatu kabla kwamba saratani yake ilikuwa imerejea. Alikuwa anajaribu kuokota vipande na kurejelea maisha yake ya kawaida. Lilikuwa jambo la kuhuzunisha sana kusoma shairi la Amanda, kwa hivyo familia ikajibu kwa mashairi matatu yafuatayo ya kutia moyo.

28 TUA MZIGO WAKO

Laura aliandika shairi hili, ili kumfariji na kumhimiza Amanda.

29 MUNGU?

Lisa aliandika shairi hili, ili kumfariji Amanda kwa kumjulisha kuwa angependa Amanda apone, lakini pia alijua kwamba Mbingu yamngoja. Ikiwa Lisa angemruhusu aende, angefanya hivyo lakini sio kwa furaha.

31 KULINGANA NA MPANGO

Babake Amanda aliandika shairi hili, ili kumfariji Amanda na kumwondolea hofu ya kifo kwa kumwomba aamini mpango wa milele wa Mungu.

32 KIGANJANI MWA MKONO WAKO

Amanda alidhani kuwa atapona na kuweza kuendelea na maisha yake, lakini akagundua kuwa alikuwa pale alipoanzia, Kiganjani mwa Mikono Yake.

33 NA BADO

Amanda alikuwa na nia thabiti ya kupona, lakini pia alikuwa na nia thabiti ya kujisalimisha kwa Mapenzi na Mpango wa Mungu kwa maisha yake; akifahamu kwamba alihitaji tu Upendo na Neema za Mungu.

34 BADO NASUBIRI

Amanda alikuwa bado anasubiri Malaika wa Mungu amchukue mbinguni. Mungu alijibu aombi yake, kwa kuwa alifariki mwezi mmoja baadaye, baada ya kuandika shairi hili.

35 UPENDO WA DADA

Shairi hili linasema ni bora kupenda na kisha kupoteza, kuliko kukosa kupenda hapo awali.Picha hii ya harusi ni ya Amanda na dada zake mapacha, Lisa na Laura.

36 USIKATE TAMAA

Amanda alipata matatizo alipokuwa akipata matibabu katika Kliniki ya Mayo huko Rochester, MN. Baba yake aliandika shairi hili ili kumtia moyo na kumtia nguvu za kustahimili safari ya ndege ya kurudi nyumbani California.

37 KUPITIA CHANGAMOTO MAISHANI, KUONGOZWA NA LENGO LA MAISHA

Shairi hili liliandikwa na Baba ya Amanda ili kumkumbusha kwamba maisha haya sio mwisho na kwamba tunahitaji kuzingatia tunakoenda baada ya pumzi yetu ya mwisho..

38 KUELEWA SARATANI BILA MUNGU

Amanda aliandika kuhusu vitu vyote alivyopoteza kutokana na saratani (mtazamo wa kiulimwengu).

39 KUUGUA SARATANI UKIWA NA MUNGU

Amanda aliandika kuhusu mambo yote aliyoyapata kutokana na saratani (mtazamo wa maisha ya milele).

Kusherehekea Maisha ya Amanda

Maneno haya yalisomwa na Tom, babake Amanda, kwenye ibada ya wafu ya Amanda.

Kwa siku chache zilizopita nimejitahidi kutafuta maneno ya kuheshimu kumbukumbu ya Amanda. Nimeomba Mungu aniongoze, lakini ni nani anayeweza kujiandaa kwa ajili ya siku kama ya leo? Je, ninawezaje kuelezea kumbukumbu za maisha kwa dakika chache tu? Ningeweza kuwaeleza kuhusu Amanda - msichana wetu mdogo, kutoka hadithi za wakati wa kulala, hadi kupoteza jino lake la kwanza, kutoka kwa michezo ya soka, hadi mashindano ya kutamka herufi za maneno, kutoka kwa kuhitimu, hadi harusi yake... au ningeweza kushiriki nanyi kuhusu imani yake ya ajabu kwa Mungu. Hatimaye, nimeamua kufanya yote mawili.

Amanda mara nyingi alitumia ushairi kueleza yaliyo moyoni na kuandika hisia zake zote. Kwa heshima ya Amanda, ningependa kuanza kwa kusoma shairi lake la kwanza, aliloandika akiwa na umri wa miaka 16, muda mfupi baada ya kutambuliwa kuwa na saratani. Kichwa chake ni - Mambo Madogo.

Je,umewahi kufunga macho yako usiku
Na kufurahia kila ndoto
Je, umewahi kutazama macho ya baba
yako Ili kuona mng'ao huo?

Je, umewahi kutembea ufukweni Na
kuhisi mchanga laini katikati mwa vidole
vyako Je, umewahi kuweka kumbukum-
bu ya tabasamu la mpendwa wako
Hadi mkunjo mdogo kwenye pua zao?

Je, umewahi kuhisi mwanga ndani yako
Ikiwaka kwa ghafla na kunang'aa sana
Au je, umefuatilia viganja vya mikono
yako Kila mstari mgumu?

Je, umewahi kuthamini mguso laini wa
mama
Alipokufunika kwa blanketi usiku Je,
umewahi kumshukuru Mungu kwa vitu
vyote vidogo Kwa marafiki, kwa maisha,
kwa uwezo wa kuona?

Tuko hapa kusherehekea maisha ya binti yetu, Amanda. Inasemekana mara nyingi kuwa watoto hawapaswi kufariki kabla ya wazazi wao na kwamba kuzika mtoto wako ni mojawapo ya matukio yenye uchungu zaidi ambayo mzazi anaweza kustahimili. Lakini, baada ya miaka 23 ya maisha, Amanda alitufundisha kwamba leo si mazishi, ni sherehe; sherehe ya maisha yake na, muhimu zaidi, sherehe ya ushindi wake dhidi ya kifo kupitia Kristo.

Amanda alizaliwa tarehe 10 Juni, 1982 maili chache tu kutoka nyumbani, huko Newport Beach. Siku hiyo, mimi na Linda hatukujua kuhusu safari ambayo tulikuwa karibu kuanza au jinsi maisha yetu yalivyokuwa karibu kubadilika milele. Amanda alikuwa mtoto wetu wa kwanza kati ya watoto wanne na akawa "msichana wa baba" kwa haraka. Linda alikuwa na wivu kidogo, lakini kuanzia wakati Amanda angeweza kutoshea kwenye kiti cha gari, tulienda naye kila mahali

nilipoenda. Tulikuwa hatutengani na alijifunza haraka kupenda magari ya kubebea mizigo na muziki wa nchi.

Sitasahau kamwe jinsi alivyokuwa akiruka kutoka kitandani kila asubuhi aliposikia mlango wa mahali pa kuegesha magari ukifunguliwa na kukimbilia dirishani na kunipungia mkono nilipokuwa nikienda kazini. Hakukosa hata siku moja. Tulikuwa hatutengani na kila siku nilikuwa na hamu sana ya kurudi nyumbani kutoka kazini ili kuwa naye. Alikuwa Shelle Belle wangu mdogo. Sikuwahi kukosa kongamano la walimu na wazazi, maonyesho ya muziki, sherehe ya utuzaji, mchezo wa soka, au tukio lingine lolote. Nilikuwa Baba anayetunza mtoto (Mr. Mom) na ninajivunia hilo. Kwangu alikuwa zambarau ya sukari nami nilikuwa fyulisi chungu kwake.

Nina kumbukumbu nyingi sana za Amanda alipokuwa akikua. Lakini, ninakumbuka pia tarehe ambayo itakuwa akilini mwangu milele. Ilikuwa tarehe 10 Novemba, 1998 na Amanda alikuwa na umri wa miaka 16 tu. Siku hiyo nilisikia maneno manne ambayo mzazi hataki kamwe kuyasikia, “Binti yako ana saratani”.

Zilikuwa habari za kuhuzunisha kwa familia nzima, lakini Amanda alikuwa mpiganaji na muhimu zaidi, alikuwa na imani yenye nguvu ajabu katika Mungu na Yesu Kristo - zawadi aliyopokea kutoka kwa mama yake. Ninakumbuka nikimpeleka nyumbani baada ya kupokea habari hizo mbaya na kuzungumza naye kuhusu matibabu ambayo yangefuata. Amanda hakuogopa kwa sababu alijua kuwa “baba angetatua kila kitu”.

Tulienda matembezi ya jioni naye na alinitazama na kusema, “Nina furaha sana kwamba nimepata saratani nikiwa na umri mdogo.” Nilishangazwa sana na maoni yake na akanieleza: “Kuugua saratani kumenifungua macho na ninaweza kuona maisha kwa uwazi zaidi sasa. Nilikuwa nikihangaikia mambo kama vile aina za nguo ambazo nimevaa au aina ya gari ambalo ningeendesha. Sasa, yote haya hayaonekani kuwa ya muhimu sana. Sitaki kutumia dakika moja ya maisha yangu kwa mawazo hasi. Watu wengi wanaishi hadi uzeeni na hawatambui kamwe mambo muhimu. Lakini nimegundua nikiwa na miaka 16 na sasa nitaishi maisha yangu yote kwa namna tofauti.” Huyo alikuwa Amanda wangu. Mara nyingi tunafikiri kwamba tunawaongoza watoto wetu, lakini kuanzia wakati huo na kuendelea, Amanda alikuwa ananiongoza.

Mashairi aliyoandika yanaonyesha ukuaji wa mara kwa mara aliopitia wakati wa vita yake ya miaka 7 dhidi yasaratani, kwani imani yake ilijaribiwa na kuimarishwa kila wakati. Amanda siku zote alitaka kukumbukwa kwa imani yake na hakuwahi kutaka kuonekana kama mhasiriwa. Alitaka Mungu amtumie Atakavyo, hata ikiwa hilo lilimaanisha kuwaonyesha wengine jinsi alivyotegemea nguvu Zake wakati wa ugonjwa wake.

Amanda aliniambia kwamba hataki kuwa Mkristo mwenye msimamo usio wazi. Alisoma Biblia kila siku na vilevile alisoma vitabu, kuomba, na kufanya masomo ya Biblia katika jitihada za kufikia kile alichokiita kiwango kinachofuata katika imani yake.

Ningependa kusoma moja ya mashairi yake ambalo linaeleza yeye alikuwa nani na alisimamia nini. Ni aina ya shairi lilaloelekezwa kwako moja kwa moja, la imani, ambapo Amanda anatetea imani yake katika Kristo. Kichwa chake ni - Kuwa na Mungu Moyoni

Unakaa pale ukisubiri bila lengo
Ukisubiri maisha yapite
Unasema huna haja na Mungu wangu
Je, unaweza kunipa sababu nzuri?

Unaniambia kuwa imani yangu ni gongo dogo la kunisaidia
Kwamba hutadanganyika kwa urahisi
Unahitaji ushahidi, thibitisho, kitu ambacho unaweza kugusa

Wengine hudai hakuna Mungu
Wakati wanapomtumikia mmoja kila siku Inachukua umbo la nafsi yao
Na kila wakati wanataka mambo yafanyike jinsi wanavyotaka

Unahisi hali ya utupu
Unakutesa ndani
Unagaagaa katika kujihurumia
Ukidhibitiwa na kiburi chako

Ukiwekeza kwenye vitu ambavyo havina maana Vitu ambavyo havitadumu
Unakataa kumpa Kristo maisha yako
Kwa sababu uliumizwa siku za nyuma

Unakataa kumtambua Mungu
Unajitenga na imani yangu
Unaishi kwa maarifa yako kuu
Wakati ninaishi kwa moyo wangu wenye furaha

Imani yangu ni kichocheo chenye nguvu
Imani yako katika nafsi yako, ni kizuizi
Unajenga maisha yako kwenye mchanga
Wakati ninashikilia Mwamba wangu wa Milele

Endelea kushikilia maarifa yako mwenyewe Na utazama binafsi
Ukijaribu kutosheleza kila kitu isipokuwa Mungu Katika shimo tupu, lililoumbwa na Mungu.

Acha kupoteza muda wako wa thamani
Bila Malengo na ukiishi kama kipofu
Toka kwenye jela ya kiburi
Ili siku hiyo Mwenyezi Mungu atakapo-toa ushahidi, ithibati, jambo ambalo huwezi kulikataa –
Hutaachwa nyuma.

Amanda Dieppa, 2004

Wengi wamehuzunika sana kuhusu Amanda na maisha magumu aliyoyaishi. Mara nyingi nilijiuliza maisha yangekuwaje kama hangekuwa mgonjwa kamwe. Lakini alithamini sana maisha yake, akiwa amejawa na upendo kwa Mungu, familia, na marafiki, na mume wake anayempenda, Aaron. Ubora wa maisha yake haukupimwa kwa idadi ya miaka aliyoishi, bali kwa kile alichotimiza katika miaka hiyo. Sisi sote tunaweza kujiuliza ikiwa maisha yetu yameleta mabadiliko kwa mtu yeyote. Kwa kuzingatia mtazamo huo, Amanda aliishi maisha kamili, alitimiza mengi sana, na akaleta mabadiliko katika maisha ya wengi kuliko watu wengi wanaoishi hadi uzeeni.

Kutoka siku ya kutambuliwa kwa saratani kwa mara ya kwanza hadi siku alipoaga dunia, Mungu alitubariki na miaka saba zaidi ya kuwa na Amanda na kwa hilo nitashukuru milele. Katika kipindi hicho tulifurahia mahafali ya shule ya upili, maadhimisho ya siku ya kuzaliwa ya 18 na 21, na niliweza kumshika mkono kuelekea jukwaani kwenye harusi yake. Hizo ni baadhi ya kumbukumbu za thamani ambazo sitawahi kusahau.

Kabla ya kifo chake, Amanda alisema kwamba ikiwa alikuwa amesaidia hata mtu mmoja kumwamini Mungu, basi miaka saba iliyopita ya maumivu na kuteseka ilikuwa yenye thamani. Ninaweza kukuambia kwamba alinielekeza kwa Mungu na kunifanya kuwa na hamu ya kuwa mtu bora na Mkristo bora. Hiyo ni sehemu ya alama aliyoiacha na itadumu ndani yangu katikamaisha yangu yote.

Amanda alishiriki matamanio yake kabla ya kufa nayo yalikuwa:

- Ningependa wimbo "Watanikumbukaje" uchezwe kwenye ibada yangu ya wafu.
- Sitaki mnisahau.
- Ningependa mashairi yangu yachapishwe na kutolewa bila malipo ili kuwatia moyo wengine na kuwaonyesha chanzo cha nguvu zangu, kutoka kwa imani yangu.
- Ningependa kumshukuru kila mtu kazini ambaye alinisaidia mimi pamoja na familia yangu kwa miaka mingi sana. Ningependa wajue kuwa nitawashukuru kila wakati kwa msaada wao.
- Ningependa familia na marafiki wangu wamkubali Kristo kama nilivyomkubali, ili nipate kuwaona wote mbinguni.

Niwazia tu jinsi Mungu anamkumbatia Amanda mbinguni na kumwambia, "Vema mtumishi wangu mwema na mwaminifu."

Ninakupeza, Amanda.
Moyoni mwangu, Nitakupenda milele.
Baba



Mambo Madogo

Je, umewahi kufunga macho yako usiku
Na kufurahia kila ndoto
Je, umewahi kutazama
machoni mwa baba yako
Ili kuona mng'ao huo?

Je, umewahi kutembea ufukweni
Na kuhisi mchanga laini katikati mwa vidole vyako Je,
umewahi Kuweka Kumbukumbu ya tabasamu
la mpendwa wako
Hadi mkunjo mdogo kwenye pua zao?

Je, umewahi kuhisi mwanga ndani yako
Ikiwaka kwa ghafla na kunang'aa sana
Au umefuatilia viganja vya mikono yako
Kila mstari mgumu?

Je,umewahi kuthamini mguso mzuri wa mama
Alipokufunika kwa blanketi usiku
Je, umewahi kumshukuru
Mungu kwa vitu vyote vidogo
Kwa Marafiki, kwa maisha, kwa
uwezo wa kuona?



Amanda Twellman, 1999



Yesu akasema, "Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie, kwa maana ufalme wa mbinguni ni wao."." **Mathayo 19:14**

Kuvunjika Moyo Kuna Baraka

Nimetosheka na maisha yangu
mazuri Ninayoishi kila siku
Nachukulia maisha kwa urahisi
Nafanya mambo kwa njia yangu

Bwana, maisha yangu hayakuwa
ya kupendeza,
Nilikuwa nimesimama tuli
Nikiteseka kwenye njia yangu
Nikipuuza mapenzi
Yako kamilifu

Nilipoteza yote
Siku hiyo yenye giza na huzuni
Mungu, Siwezi kuacha kulia
Usiondoe yote

Kila siku nasubiri
Nikiwa na maswali mengi akilini
mwangu
Bwana ananipa majibu
Baba, nimekuwa kipofu sana

Nilipokuwa kwenye giza kuu Bado
ananivuta karibu naye
Mtoto wangu nimekuwa
nikikuita
Mungu, sikusikia

Ninazama polepole
Ninalia kila usiku
Bwana, nahitaji nguvu zako
Je, anasikia shida zangu kweli?

Lakini Ananinyanyua
Huku akinifuta vumbi mgongoni
Ananijaza na matumaini
Na imani ambayo nimepungukiwa
nayo

Bwana, inazidi kuwa ngumu
Nashindwa kustahimili Lakini
Yupo kando yangu
Kwa hivyo ninapata nguvu ya
kuendelea

Mungu nimepiga magoti
Unaliita jina langu kwa sauti ndogo
Umenipa maisha mapya
Sitabaki jinsi nilivyo

Umewasha moyo wangu kwa moto
Umenikomboa kwa neema Yako
Upendo wako ni kama mafuriko -
Mungu, nauona uso Wako

– Amanda Twellman, Juni 2002



Ee Bwana, umenichunguza na kunijua!
***Zaburi* 139:1**

Baraka Zisizo Tarajiwa

Uso kwa uso na Muumba wangu
Macho yangu nimeyafumbua sana
Vipande vipya vyangu vinapata uhai
Lakini vipi kuhusu vile vilivyo kufa?

Nikijua jinsi ninapaswa kuhisi,
Najikaza akilini mwangu
Taratibu, napiga hatua mbele, nashikilia pumzi
Nikitazama nyuma kuona nilicho kiacha

Macho yote yameelekezwa kwangu
Wakisubiri kuona nitakachofanya
Ninatupilia mbali ya kale kwa kusitasita
Na Mungu ananikabidhi maisha mapya kwa fahari

Maisha haya mapya ni yenye nguvu, furaha, yaliyokomaa
Zaidi ya nilivyowahi kuota
Niko tayari kulenga mbele
Au angalau, kwa hivyo ilivyonekana…

Wakati mwingine mimi hukosa siku nzuri za zamani,
Nimeupoteza unyoofu kama wa mtoto


Lakini badala yake alinipa imani yenye utulivu,
Akijua kuwa ilikuwa na thamani ya gharama

Kwa hivyo ninapohisi kama ninazama katika ulimwengu huu,
Nikijaribu kutosheka na kidogo Nitageuka na kuinua macho yangu
Kwa Yule pekee ninayependa kumpendeza.

Amanda Twellman, 29/11/02

Siku Bora Zaidi

ninafumba macho yangu
ninazama kwenye
mawazo ya siku bora zaidi ya
siku za nyuma ninayo
ikumbuka ninaota kuhusu
maisha ya siku zijazo chochote
kisipokuwa maisha ya sasa
mara nyingi ninahisi ni dhaifu
mwenye uchovu
aliyechanganyikiwa kwa kukata
tamaa
Niko karibu kukata tamaa lakini
kupigania mustakabali wangu
ndicho kitu
ambacho kinanipa ujasiri siku
nzima ninaweka tabasamu
langu najifanya hainiumizi na
najitia nguvu niwezavyo
lakini hakuna mtu anayejua
ukweli usiku wakati
ninayaruhusu machozi
yanitoke nikiwa peke yangu
nainamisha uso wangu
siyakaushi wala kuyazuia
ninamlilia Mungu na kumsihi
anirejeshee maisha yangu ya
zamani
kila mtu anayetaka
kunisaidia yuko radhi
kunishika mkono





lakini hakuna anayeelewa
vizuri jinsi ninanavyohisi…
nywele zangu
zinaendelea kukatika
nahisi mwili wangu
haupendezi sana
ninahisi mwili huu si wangu,
siwezi kupanga
maisha yangu ya
baadaye najihisi
dhaifu sana
ninahisi kana
kwamba sina uhai
moyo wangu
unauma
machozi hayatoki
machoni mwangu tena
nachukia hili
ninachukia vile hali
hii inavyoathiri
familia yangu,
mwenzi wangu
wa roho,
marafiki zangu
naomba sana hali hii
iishe hivi karibuni
uniondolee
Mungu, naomba unipe nguvu
usiniache
Hadi pale mawazo ya siku
bora sio mawazo tu

Amanda Twellman
29/12/02

Si Jibu Nililotarajia

Napiga magoti kila usiku
Nikikusihi kwa maombi yale yale
Nikiwa na tumaini la jibu moja tu
Uchungu wa kusubiri unanishinda kustahimili

Hatimaye jibu Lako linakuja
Lililo wazi na lisilopingika
Lakini sio lile nililotarajia, Mungu
Na mwanzoni nimejawa na hofu

Kwa huzuni ya muda mfupi, ninatokwa na
machozi mengi yanayofuatwa na mashaka
Mungu, mpango Wako ni upi?
Nilikuwa na uhakika kwamba ungenisaidia

Kisha Anazungumza na moyo wangu kwa upole
Anafichua mapenzi
Yake kamili Udhaifu wangu wa kudumu unaleta
utukufu kwa nguvu
Zake Kwa hivyo kwa hofu nasubiri

Ninaamka kila asubuhi
Nikiwa na tabasamu kubwa zaidi usoni mwangu
Sina uhakika kabisa kuhusu kesho
Lakini siku zote nina imani katika neema yake

Kwa hivyo sitapoteza imani
Kwa kuwa ananifundisha kustahimili
Hata katika majaribu nimejawa na furaha nyingi
Kwa kuwa ninajua siku moja tukufu
Atanifuta kila chozi!

Neema yangu yakutosha, maana
uweza wangu hutimilika katika udhaifu.
2 Wakorintho 12:9

Amanda Twellman
16/01/2003

KUVUMILIA KATIKA MAOMBI



Nimechoka na kuvunjika kabisa
Nimedhoofika kutokana na dhoruba
Nikipambana kuvumilia katika maombi
Nimechoka na kuishiwa na Imani

Ninapambana kuwa jasiri
Je, mstari wa kumalizia unasonga mbele zaidi?
Nimeinua macho yangu kwa maswali kwa
mbingu zilizo kimya
Lakini midomo yangu haiachi kuomba

Anaponifinyanga kwa kusudi
Lake Imani yangu inaimarishwa
Ghafla kila wingu jeusi
Limepambwa kwa fedha nyingi

Siogopi tena yajayo
Wala mambo yaliyo nje ya uwezo wangu
Nazingatia yale ya milele
Hali ya nafsi yangu

Kisha...

Jibu ambalo nilitarajia
Kwa maombi niliyoanza kitambo
Ninasimama kwa kicho tu bila la kusema
Nikifurahia mwanga

Nainua macho yangu mbinguni
Ninapokuwa na shukrani na sio wakati nanapokuwa na uoga tu
Kwa kushangazwa ninaanguka chini kwa magoti yangu
Kwa maana nimeumbwa kwa namna ya kutisha na ya ajabu

Kuishi maisha kama fursa niliyopewa bila kustahili
Ghafla kunaleta maana kamili
Nikingoja alichopanga
Nikitabasamu kwa taharuki nzuri

limeandikwa na: Amanda Twellman, 09/01/2003



Shughuli Nyingi Maishani



Umeshikwa na shughuli nyingi
Unaamka kila siku
Je, una wakati wa kutoa shukrani kweli
Je, una muda wa kuomba?

Umezidiwa na mafadhaiko Majaribu yanapokujia
Wasiwasi hauwezi kukuongoza
Ikiwa una imani ya kuomba

Ukiangazia macho siku zijazo
Na kusahau kufurahia ya siku ya leo
Ya kale yamepita, umesamehewa
Chukua muda, vuta pumzi, na uombe

Unafanya kazi kwa kimya Ukisubiri siku hiyo
Vema, mtumishi wangu mwema na mwaminifu...
Yatakuwa maneno yake kwako

Amanda Twellman
18/09/03

Ahadi Zisizotimizwa

Amanda Dieppa, 2003

Wakati kila kitu kinakwenda sawa
Na nina siku nzuri
Ni rahisi jinsi gani kukusifu
Na kuomba kwa furaha

Polepole ninakusahau
"Ninaweza kufanya haya peke yangu"
Upweke unaingia polepole
Na ninaanza kuhisi niko peke yangu

Mara kwa mara Unabisha
Lakini moyo wangu haukuruhusu kuingia
Kwa sababu sina utulivu
Na dhiki na dhambi ya ubinafsi

Nina uvivu sana na ukaidi sana
Kukubali kuwa mimi ni dhaifu
Badala yake natangatanga gizani
Wakati ni Wewe ninayehitaji kumtafuta

Ninaibeba mizigo yangu mwenyewe
Mzito sana, naanguka na kujikwaa
Kwa huzuni, ninasubiri hadi nianguke kifudifudi
Ili niweze kujifundisha kuwa mnyenyekevu

Njia ya maisha imegeuka kuwa mbaya na yenye changamoto nyingi
Na nina siku mbaya sana
Je, nimemkasirikia Mungu
Kwa kuruhusu nipatwe na shida?

Kisha nafikiri kuhusu ahadi zake
Za maisha ya milele Ametimiza zote
Alisema hataniacha kamwe
Lakini hakuniahidi kuwa sitaanguka

Ataniongoza nipitiapo kwenye miale ya moto
Atanipa nguvu za kushinda
Nikiwa peke yangu siwezi kwenda popote
Nikiwa na Kristo naweza kwenda mbali

Kwa hivyo wakati kila kitu kinakwenda mrama
Na ninakabiliwa na changamoto nyingi
Mungu mwenye upendo, mwaminifu huniongoza
Ndiye anayestahili kusifiwa milele!



Nimepoteza Vyote

Nimekufa moyo na kukosa la kusema maishani
Ninahisi moyo wangu umevunjika kabisa
Maisha yalionekana kuwa dhabiti sana, kamili
Hadi matumaini yangu yalipokatizwa

Nikabaki nikihisi sina chochote
Imani yangu imetikiswa
Nimeganda kwa woga na kuchanganyikiwa
Ghafla sina chochote, nahisi nimeachwa peke yangu

Moyoni ninajua ukweli
Upendo wake upo siku zote
Lakini sehemu yangu hulia kwa mafadhaiko
Kwa sababu maisha sio sawa

Ninajitahidi kuwa kielelezo
Nimepungukiwa kabisa kufikia
Ninaanguka chini kwa kukata tamaa
Nikihisi kama aliye gizani

Lakini mwale kidogo ya imani
Polepole huingia akilini
mwangu Imekuzwa katika
majaribio ya maisha yangu ya
nyuma Inaboreshwa kila mara

Nimepoteza kila kitu
Imani, ndicho kitu cha pekee ambacho
nimesalia nacho mkononi mwangu
Nina furaha isiyotegemea kitu kingine
chochote
Kumaliza mwendo na kusimama imara

Amanda Dieppa 26/02/04



Kikombe Kilichojaa Pomoni

Nimechoka sana na maisha haya
Bwana, niruhusu nikate tamaa
Niondolee uchungu
Niondolee matatizo yangu

Uchungu wa nafsi yangu
Bado nauhisi ndani yangu
Nazuia mito ya machozi
Siruhusiwi kulia

Udhaifu wa kibinadamu
unanishinda
Nimepofushwa na hisia
Ninazama katika maisha
yasiyoeleweka, Bahari iliyochafuka

Uso wangu, una tabasamu ya kinafiki
Unasaliti kilicho ndani yangu
Moyo wangu, umevunjika kutokana na kukata tamaa
Napigana vita nisivyoweza kushinda

Nisaidie, wewe ndiwe tumaini langu la pekee
Wewe ni yule yule leo, jana, kesho
Usiruhusu mwanga ndani yangu
Uzimike katika wimbi la huzuni

Imani yangu ya kuendelea ilimedhoofika sana
Ujasiri wangu wote umeisha
Lakini naamini, natumaini, nasubiri
Siku moja…
Atakapojaza kikombe changu hadi kifurike



Amanda Dieppa
3/3/04

KUWA na MUNGU MOYONI

Limeandikwa na Amanda Dieppa 24/03/04

Unakaa pale unangoja bila malengo
Ukiruhusu maisha yapite
Unasema huna haja na mungu wangu
Je, unaweza kunipa sababu nzuri?

Unaniambia kuwa imani yangu ni
gongo dogo la kunisaidia
Kwamba hutadanganyika kwa urahisi
Unahitaji ushahidi, thibitisho,
kitu ambacho unaweza kugusa

Wengine hudai hakuna Mungu
Wakati wanapomtumikia mmoja kila siku
Inachukua umbo la nafsi yao
Na kila wakati wanataka mambo
yafanyike jinsi wanavyotaka

Unahisi hali ya utupu
Unakutesa ndani
Unagaagaa katika kujihurumia
Ukidhibitiwa na kiburi chako

Ukiwekeza kwenye vitu ambavyo havina maana
Vitu ambavyo havitadumu
Unakataa kumpa Kristo maisha yako Kwa
sababu uliumizwa siku za nyuma




Unakataa kumtambua Mungu
Unajitenga na imani yangu
Unaishi kwa maarifa yako kuu
Wakati ninaishi kwa moyo wangu wenye furaha

Imani yangu ni kichocheo chenye nguvu Imani
yako katika nafsi yako, ni kizuizi
Unajenga maisha yako juu ya mchanga
Ninaposhikilia Mwamba wangu wa Milele

Endelea kushikilia maarifa yako
mwenyewe Na utazama binafsi
Ukijaribu kutosheleza kila kitu
isipokuwa Mungu Katika shimo
tupu, lililoumbwa na Mungu.

Acha kupoteza muda wako wa thamani
Bila Malengo na ukiishi kama kipofu
Toka kwenye jela ya kiburi
Ili siku hiyo Mwenyezi Mungu atakapotoa ushahidi,
ithibati, jambo ambalo huwezi kulikataa –
Hutaachwa nyuma.



Kuendelea Kujisalimisha

Muda mrefu sana uliopita
Nilimpa Mungu maisha yangu
Kwa kufahamu mapungufu yangu
Ninakumbuka vizuri sana

Nikampa udhibiti kamili
Nikiwa na uhakika katika utunzaji
Wake Nikitegemea nguvu Zake
Hakuna uzito ambao nisingeweza kustahimili

Lakini kwa namna fulani ninaanza
kutoka polepole
Kutoka kwa macho Yake yenye thamani
Nikachukua kile nilichokuwa nimempa
Nikaubeba mzigo ambao sio mwepesi tena

Nimekwama katika mzunguko usio na mwisho
Maisha haya yanachanganya sana, ni magumu
Udhaifu wangu wa kila mara, kutokamilika
Kunaniacha nikiwa nimechanganyikiwa na
kukata tamaa

Lakini Bwana anangoja kwa upendo
Ananisubiri ninapofanya uamuzi wangu
Hunihakikishia kila wakati kwamba
Mimi sio mtu asiye na tumaini.

Limeandikwa na Amanda Dieppa 16/06/2004

WAKATI WA KUKATA TAMAA

Ninapata nini ninapoona maisha yangu?
Najihisi asiye na tumaini na aliyejawa na huzuni
Ninapata nini ninapoona yale yanayotendeka karibu nami?
Nina huzuni na ninahofia kesho

Ikiwa maisha haya ni jaribio kweli
ninaogopa kuwa ninaanguka sana-
Ni dhaifu sana, nimechanganyikiwa,
ninapotea mvua inaponyesha…
Na sasa kunanyesha mvua ya mawe bila kukoma

Na ninapogonga mwamba
Wengine hujaribu kunimaliza
Wananigeuzia migongo yao,
wananipuuza
Ninazama taratibu peke yangu

Nipo katika wakati huu wa kukata tamaa
Nimepofushwa na machozi yanayotiririka
Nini hutokea ninapomtazama Yeye?
Ananielewa na Anasikia

Ananipa tumaini la milele
Ninaweza kutegemea familia na marafiki
Faraja ya pekee
Maisha haya sio mwisho

Amanda Dieppa, 18/06/04

Baada Ya Muda Mfupi

Ninatoa shukrani, shukrani, shukrani
Kwa baraka zinazomiminika
Ingawa sistahili hata mmoja
Ninahisi upendo wake na ninajua

Nina pendwa, pendwa, pendwa
Kama nyota yake nataka ning'ae,
Anionapo, atabasamu, na kusema
Mtoto, wewe ni Wangu!

Hivyo nimejawa, nimejawa, nemejawa
Na furaha yake na kwa Roho Mtakatifu
Nauona utukufu wake kamili
Na nina hamu kubwa ya kuuonyesha kwa wengine

Nina amani amani, amani
Nikijua kuwa Yeye Ndiye Anayetawala Ninaishi maisha
Aliyopanga kwa njia ya kipekee sana
Muumbaji wa nafsi yangu.

Nasubiri, nasubiri, nasubiri
Kwa Bwana wangu atimize ahadi
Yake Nikiwa na matumaini yakini
Baada ya muda mfupi

Limeandikwa na Amanda Dieppa,
14/07/04



Yafungue Macho Yangu

Nimepofushwa kwa machozi
Nimepofushwa na hofu
Yaonekana hakuna njia ya kutoka
Nimefungiwa kwenye mtego
Ninahema kwa pumzi kubwa
Ni dhaifu sana kupiga kelele au kupiga mayowe

Moyo na roho yangu haina nguvu
Ninahisi kwamba imani yangu imeisha
Ninalia tena Na tena
"Tafadhali niondolee kikombe hiki"

Muda unapita upesi
Siku zinapita kwa haraka
Dunia inasonga huku nikiwa nimesimama tuli
Niokoe kutoka kwenye mtego huu
Niondolee maumivu haya
Yafumbue macho yangu ili nione
Mapenzi yako ya ajabu

Ninaanguka chini
Na kusimama tena
Kisha kuangushwa tena
Ninapoteza mbio hizi Ninapoteza akili yangu
Je, kunaweza kuwa na njia ambayo ninaweza
kupata ushindi?
Imani yangu inaisha Matumaini yanafifia
Ingawa ninapambana kuishikilia kwa karibu

Mbona uko mbali nami
Mbona umenyamaza
Wakati ninakuhitaji sana?

Uliiumba nafsi hii
Ukaiipa uhai
Ndio maana najiuliza mbona
Nimechanganyikiwa, mbona nimekasirika
Nina wasiwasi na nimevunjika moyo
Je, kuna njia nyingine yoyote?

Moyo unawaka moto
Imani isiyotikisika
Wakati moja nilikuwa nimechochewa
Sasa nimebaki
Na utupu
Na sina mahali pa kujificha

Niondolee,
Niondolee
Tafadhali, tafadhali sikia kilio
changu
Chochote kile
Unachopanga kufanya---
Yafungue macho yangu.



Amanda Dieppa
27/12/2004

Yesu akasema, "Nimekuja ulimwenguni kutoa hukumu, ili wale walio vipofu wapate kuona..."
***Yohana* 9:39**

Utele



Hisia ya utele imejaa nafsini
mwangu
Moyo wangu hauna hofu tena
ninahisi kamili na mzima

Ubatili wa maisha
Sasa umebadilishwa ghafla
Kwa hisia kubwa ya kusudi
Na sina wakati wa kupoteza

Kabla sijazaliwa

Nilikuwa katika Mpango Wako
Mawazo yako ya upendo kunihusu
Yanazidi mchanga

Kwa hivyo ninajitahidi kuishi
maisha yenye maana
Na kukataa kutosheka na kidogo
Ninajitolea kufanya sehemu yangu
Nikijua Utafanya mengine

Amanda Dieppa, 24/01/2005

Eeh Mungu, fikira zako zina thamani nyingi kwangu!
...Kama ningezihesabu ni nyingi kuliko mchanga.
***Zaburi* 139:17-18**

MAJARIBU YA MUDA MFUPI

Jaribio baada ya jaribio
Nimebanwa kila upande
Nikivumilia kimya kimya
Mtihani mwingine wa maisha

Siku baada ya siku
Ninajitahidi na ninajaribu
Kukabiliana na matatizo ya
muda Mfupi bila kuuliza, "Mbona?"

Msimu baada ya msimu
Ninapitia nyakati za furaha na za
Huzuni ikiwa nitafaulu au sitafaulu
Imani yangu inakua kila wakati

Muda baada ya muda
Imani yangu inakuwa vuguvugu
Kisha inachochewa tena
Unapokutana nami katika dhoruba

Ushindi baada ya ushindi
Ninakupa utukufu wote
Kila hitaji ambalo nimewahi kuwa nalo
Umeliona na umekutana nalo

Amanda Dieppa
02/02/2005

MATUMAINI YASIYO NA MWISHO



Ninakosa pumzi kutokana
na hofu
Siwezi kuhisi moyo wangu
Ninapozitazama ndoto zangu
Zikiporomoka, zikikosa kutimia

Vita vile vile ambavyo
Nimepigana kwa miaka
Hofu yangu kuu, hali halisi
Jibu langu la pekee, machozi

Ningali mwenye nguvu katika Kristo
Bado udhaifu wangu unaonekana
Wakati tegemeo langu ni kwake
Na hakuna ninachoweza kufanya

Kwa muda mfupi tu mimi ni dhaifu
Kisha ninapata imani
Ninajua kuwa niko mikononi Mwake
Hapo ndipo nimekuwa siku zote

Niondolee kila kitu
Hata nikabiliane na kifo -
Nitasema kwamba Mungu ni mwema
Kwa pumzi yangu ya mwisho kabisa

Maisha yangu ni mafupi na ya kupita
Lakini tumaini langu halitakufa
Haijalishi kile kitakachotokea,
sitasahau...
Ni Yeye ninayemtukuza

Amanda Dieppa 07/02/2005

Nina Mzigo wa Milele

Nisaidie kuelewa, Mungu
Ninaogopa kukuuliza sababu
Kwa nini kuna uchungu mwingi,
Bwana kiasi cha kunifanya nilie?

Uso wangu umejawa na madoa ya machozi
Nami natweta kwa pumzi ya hewa
Ninahisi nimenaswa na kulemewa milele
Kwa mengi sana ambayo ni vigumu kubeba

Licha ya juhudi zangu zote
Kukumbuka kuwa Wewe upo
Bado napatwa na shinikizo
Bado ninakata tamaa

Akili zangu zinaniambia "tulia"
Lakini moyo wangu unapiga mayowe ndani yangu
Umechoka kuumizwa
Na unasema sitashinda kamwe

Huzuni imekuwa jambo la kawaida sana kwangu
Ninahisi tumaini lipo mbali nami
Nimelemewa na maisha haya
ninaogopa hata kuomba



Najua una mpango
Lakini ninaogopa kuishi kulingana na mpango huo
Ninataka kugeuka
Na kuwa na mashaka

Nisaidie kuamini, Mungu
Ninaogopa kukosa kutimiza matarajio yako kwangu
Ninaaibika kama nitawahi kushikilia
Kwa hiyo kimya nazama

Amanda Dieppa
25/02/2005

Umtwike Bwana mzigo wako naye atakutegemeza. ***Zaburi* 55:22**

Okota Vipande

Maisha yangu yanaangaza mbele yangu
Ninatazama pande zote
Vipande vya nafsi yangu iliyovunjika
vimetapakaa pande zote

Ninajaribu kuvichukua
Ili kuvirudisha mahali pake
Wakati siwezi tu kufanya hivyo
Ninalala hapo kwa aibu

Imani yangu thabiti Imesawazishwa
Mbele ya macho yangu
Hakuna wakati wa kuishi kwa unafiki
Maumivu hayawezi kufijicha

Wakati moja nilikuwa na nguvu kama
mwamba
Nimepoteza nguvu polepole
Nimepunguzwa hadi kuwa kokoto ndogo
Sina mahali pa kukimbilia

Bwana, ndani ya moyo wangu
ninakuhisi
Lakini roho yangu inahisi upweke
Mateso katika ulimwengu huu
Yanaifanya kulia na kuugua.

Tafadhali okata vipande
Unifanye niwe mpya
Nifundishe kutulia
Kukutwika fadhaa zangu

Amanda Dieppa 28/02/2005

Shairi la Amanda, kutoka kwa dada yake Laura.



Tua Mizigo Yako

Wakati maisha yako yanaangaza mbele yako,
Hakuna haja ya kutazama pande zote
Ukiwa na Mwenyezi Mungu,
Katika familia faraja yako hupatikana.
Tua mizigo yako,
Usiruhusu mizigo hii ikuumize,
Nipigie simu na ujue nitakuwepo,
li kukusaidia kwa kile unachokabiliana nacho.
Mimi ndiye ninayejawa na fedheha,
Ninapoona kuwa nina uwezo wa kufanya
kidogo sana.
Lakini ninajua kuwa una imani tele,
Unasaidia familia nzima.
Ninajivunia mafanikio yako,
Na jinsi umekuwa mwenye nguvu siku zote,
Ingawa unajiona kama kokoto,
Hiyo inanifanya nini basi?
Vumbi kidogo mbele yako,
Najitokea kuwa hapo wakati unanihitaji.
Tafadhali usihisi kama uko peke yako Amanda.
Najua sijawa dada ambaye ulitarajia niwe,
Lakini nataka kukujulisha kuwa nakupenda sana,
Na ikiwa ningekuwa na nguvu kama wewe,
Ningekuwa msaidizi na Mkristo bora, Ningekuwa.

Laura Twellman 28/02/2005



Mungu?

Siwezi kupumua
Ninapumua kwa shida huku
nimeshikilia machozi.
Je, nitaficha machozi yangu hadi lini
Na kujaribu kukataa kulia?

Maisha yanafumuka
Uzi mmoja baada ya mwingine
Upesi na haraka zaidi
Nimeanza kutulia.

Ninatafuta majibu
Yanakuwa vigumu kupata
Hivi karibuni
Nitakuwa mwenye huzuni nyingi.

Ninahisi kwamba sina shukrani
Je, ninalalamika mara kwa mara?
Mwezi mmoja haujapita
Nilikuwa nahisi vizuri kabisa.

Tazama jinsi mambo
yanavyobadilika na kuwa
machungu haraka, hatima ya
maisha yangu ni gani?

Ninahisi kwamba ninapoteza
uthibiti wa hisia zangu,
Sipendi kuwa kwenye hali hii
ya kutofahamu.

Shetani ananipangia maisha mengine kwa ustadi,
Anaweka upya maisha yangu kwa haraka,
Ananishonea mashaka na kutokuwa na uhakika
Ninahisi kama ninapoteza mbio za maisha.

Sina uwezo, ninapambana kushikilia
Tafadhali niokoe Bwana Yesu,
Kila kitu kinaenda mrama.

Imekuwa vigumu kuvumilia kazi,
Nakumbana na kukata tamaa kila siku,
Nipe subira, maisha yangu ni mabaya sana
Uchungu kidogo tu na ninaanza kuondoka.

Nimechanganyikiwa kwenye njia panda,
Nichukue njia ipi?
Nimekwama katikati,
Ninaogopa kufanya makosa.

Uzito huu kwenye mabega yangu
Ni mzito sana kuubeba
Ninazama kwenye mchanga mwepesi
Mungu uko wapi?

Nakupa mzigo wangu
Tafadhali Bwana, chukua wote.
Ninaishiwa na nguvu ewe
Mungu ninaogopa nitaanguka.

Nimesikia kuwa nikiomba,
Nami niitapewa,
Ni kazi ngumu zaidi kufanya
Kuliko vile ningeamini.

Sawa yachukue…
Ninafumba macho kwa taharuki.
Je, maombi yangu hayakukufikia?
Maisha hayana maana.

Nataka kukupa wasiwasi wangu,
Nifanye nini zaidi?
Najua ninakosa kitu fulani
Ninachokuomba ...

"Nuru hii iko wapi, Katika handaki hili?"
Nimepofushwa
"Nikikupa uchungu wangu,
Je, utanisaidia kuipata?"

Kuchanganyikiwa si kitu
Hisia hii siwezi kuelezea Inachoma ndani yangu
Chanzo cha maumivu ya mara kwa mara.

Nadhani ni moyo wangu,
Imevunjwa mara nyingi sana,
Nitafuata ushauri wa dada yangu,
Na kutatua kwa mashairi.

Ninaweza kuhisi katika familia yangu
Hamu kubwa ya amani
Kuhangaika kila siku kutafuta kitu
Ili kukomesha maumivu yao.

Pumzi nzito hutolewa kila wakati,
Ishara ya kushindwa,
Hatuwezi kueleza kwa maneno
Tunaanguka miguuni pako.

Tumaini letu liko kwako ewe Mungu,
Unajua unachofanya
Lakini tunatamani kupata majibu
Kwa maumivu tunayopitia.

Kwa nini sisi?
Kwa nini sasa?

Kamwe Simkani Mungu - Ninamuuliza Maswali Tu

Bado hatujajifunza nini?
Najua majibu yanatungoja
Mbinguni
Tutapitia maisha haya magumu
Tukitegemea uaminifu tu.

Kuitegemea imani
Ni jambo lilio gumu kufanya
Nisaidie niwe imara
Na kukutazamia Wewe.

Imani iliyo kama mbegu ya haradali
Hiyo tu ndio niliyo nayo
Hiyo tu ndiyo Unayohitaji
Na yote niliyoleta kwako.

Ningependa kuleta zaidi
Na wakati mwingine mimi huleta
Nikiwa nimeshikilia kwa nguvu
sana kwenye mikono yangu,
Lakini inaonekana bado inaanguka.

Nimekulilia hapo awali
Kuhusu yale yanayotesa moyo
wangu Kwa nini nakulilia usiku
Peke yangu gizani.

Ninawaza kila mara
Ninabishana akilini mwangu
Napambana na ukweli ulio mbele yangu
Na kuuliza maswali kwa mwenyezi mungu.

Najaribu kuelewa mambo
Ambayo yanazidi uwezo wangu
Kwa nini unafanya mambo
Na kutupitisha kwenye miale ya moto.

Una mpango
Ulioundwa kwa ajili yetu sote
Ninajua kwamba unanisikia
Unajibu maombi yangu.

Nilichagua kutozisikia
Si kwa wakati huu
Uko katika harakati za kuchagua kadi
Na ninahofia nitapata kadi gani.

Kuna kitu kimoja
Ninachotamani kwa siri,
Natamani dada yangu
Kutomaliza safari yake.

Ninatumainia nafsini mwangu
Ninaomba kwa siri
Kusudi lako kwake
Halijakamilika.

Natumaini Unamhitaji hapa
Kwa muda mrefu
Usimpeleke kwenye ulimwengu wako
Ninamhitaji katika ulimwengu wangu.

Ninaogopa jinsi nitachukulia habari hio
Kama Ungesema kuwa amemaliza safari yake
Kama Ungemchukua kutoka kwetu
Na ukasema “Nitafanya hivyo”.

Hivyo ndivyo ninavyofikiri wakati mwingine
Katika kina cha moyo wangu
Katika nyakati hizo za udhaifu
Ambazo huniathiri kabisa.

Katika kina cha roho yangu
Kwa undani zaidi kuliko msimamo huu wa kibinafsi
Ninaona zaidi ya hofu ya kumpoteza,
Kwa kusita kwangu.

Zaidi ya hisia nilizonazo
Ambazo natamani sana abaki nami,
Natumainia Mungu,
Utampeleka hadi mbinguni
Kwa sababu atakuwa sawa.

Hakuna maumivu na mateso tena
Hilo ni jambo ambalo najua utampa
Lakini zaidi ya kupata mwili mpya,
Ni kile alichokusudiwa.

Hapa sipo mahali ninapopaswa kuwa
Ningefurahia sana kuungana na
Wewe na kuwa huru
Ikiwa ana nafasi ya kufikia
lengo hilo haitakuwa ni
mimi nitakayezuia roho yake.

Tulikusudiwa kupata kitu bora zaidi
Mbinguni ndipo mahali tunapopaswa kuwa.
Kwa hivyo ikiwa lazima aende, nitamruhusu,
Sio kwa furaha tu.

Lisa Twellman, 28/02/2005

Kulingana na Mpango

limeandikwa na Baba: 28/02/2005





Je, ingekuwaje
Kuishi maisha bila maumivu
Kwenye mwili wa kiroho
Bila kasoro au doa



Kiwavi anajuaje anapokuwa
kwenye kifukofuko
Kwamba hatimaye atakuwa kipepeo
Ambaye anaweza kupepea kwa furaha



Mungu ana mpango
Lakini hofu inanipofusha
Kutoka kwa uzuri na utukufu
Wa mwili mpya wa kiungu

Nitapeana mwili wangu wa duniani
Kwani ule uliotengenezwa na mkono
Wake
Unangoja kuwasili kwangu
Kulingana na mpango

Basi kwanini ninaogopa
Na kulia kwa dhiki
Je, Mungu yupo kwa kweli
Je, maisha ni mtihani tu

Ninaomba na ninajitahidi
Lakini ninaendelea kukua
Karibu na Wewe Bwana
Na joto la mng'ao wako

Nina wasiwasi na msisimko
Kuona kile kilicho kwenye mbingu kwa
ajili yangu
Mwili mkamilifu wa kiroho
na mengi zaidi

Wale wanaoamini
Wanapata amani ya kweli ya ndani
Inayoshinda hofu zote za kifo na
magonjwa

Siku moja sote tunaaga dunia
Kila mtoto, mwanamke na mwanaume
Kwa hiyo ishi maisha yako kwa hekima
Kulingana na mpango wake

Kiganjani Mwa Mkono Wako


Ulimwengu ulikuwa wangu
Nilikuwa nimepanga kila kitu
Maeneo ya kuenda
Watu wa kuona
Nilizishika zote mkononi mwangu

Sikujua nilikuwa
Sifahamu ukweli wote
Kuna majaribu ya kukabiliana nayo
Imani ya kukuza
Safari ndefu iliyo mbele, ndefu na ya kuchosha

Kwa hiyo nilipigana vita vilivyo
vizuri Na nikafikiri kwamba nimeshinda
Tayari kuishi
Nilipogeuka ili kuendelea na maisha
Ndipo nilitambua kuwa, nimeanza tu

Ulimwengu huu, sio wangu
Umepanga kila kitu
Ningali na maswali mengi
Imani bado inazidi kukua
Ninapumzika kiganjani mwa
mkono Wako

Amanda Dieppa
07/04/2005



Na Bado

Sina shaka kamwe kwa kuwa
Wewe ndiye unaye ongoza maisha yangu
Bado kuna kitu kinawaka ndani ya roho yangu
Nia yangu ya kuishi
Unaendelea kuwaka
Unakataa kupungua

Mapenzi yako yatimizwe- bado
Lakini nina ndoto nyingi, majuto mengi
Sikukusudia kupoteza Kila siku yenye thamani
Nikifuata mapenzi yangu
Nikienda mbali na mapenzi yako

Sasa saa inaendelea kusonga
Na ningetoa chochote ili nisiwe mgonjwa
Ninaomba na kusihi
Nipate uponyaji tu
Wakati fulani ninaogopa
Hatima yangu ishaamuliwa

Tafadhali usinichukue, angalau si sasa
Nimebarikiwa na mengi,
maisha yangu ya baadaye
yamepangwa
Ujana wangu unalia
Moyo wangu
unawaka moto…

Lakini subiri---
Upendo wako ndio
ninauohitaji.

Amanda Dieppa
20/04/2005



Bado Nasubiri

Kwa nini, Bwana, kwa nini?
Ninapigana kwa muda mrefu na kwa bidii Ili kupata
angalau inchi moja tu
Na kurudishwa katika hali yangu ya kwanza?

Wapi, Bwana, Wapi
Ninapoweza kukimbilia na kujificha kwa usalama
Ili tu niondoke
Kutoka kwa mwiba huu ulio upande wangu?

Ni lini, Bwana, ni lini
Jinamizi hili litaisha?
Ninasubiri malaika
Nina hofu kuwa hutawahi kumtuma.

Vipi, Bwana, vipi
unaruhusu maumivu mengi
Ninapolia kwa imani
Na wewe unayaacha yabaki tu?

Nimgeukie nani
Ninapohisi kama haupo nami?
Nifanyeje
Ninapohisi ni kama Hujali?

Bado namsubiri malaika huyo
Lakini mashaka yatatoweka
polepole
Kutoka kwa moyo ambao
ulikuwa wenye furaha
Unaotamani Siku hiyo

Amanda Dieppa
13/06/2005





Upendo wa Dada

Je, ni bora kupenda na kupoteza kuliko kutowahi kupenda kabisa?
Je, ninawezaje kuthubutu kutoa moyo wangu wote nikijua nafasi yake ni ndogo sana?
Je! haingekuwa rahisi kutokaribia, kulinda moyo wangu ulio kwenye hatari,
Ili ikiwa ataondoka, roho yangu isivunjike sana?
Inauma sana tayari kwa sababu nimejiruhusu nikaribie
Ikiwa inaniuma kumuona akiwa mgonjwa, itakuwaje akiondoka?
Alipougua mara ya kwanza nilikimbia kwa sababu niliogopa kuwa na ukaribu,
Nilifikiri ningeweza kujiokoa kwa kupunguza kiwango cha huzuni kiletwacho na majonzi.
Niliambiwa ningejuta ikiwa singemjua vizuri zaidi, Kumpenda akiwa bado yupo hapa duniani, kila dakika yenye thamani.
Nilisikiliza wale ambao nilifikiri wanajua zaidi, kutoka kwa wale ambao walikuwa wamepoteza wapendwa wao hapo awali.
Kwa hivyo nimempenda dada yangu kwa moyo wangu wote, upendo wote niliokuwa nao. Kwa hivyo sasa ninaenda kulala usiku, nikiomba ataona kesho,
Natumai Mungu atanusuru maisha yake ili kuniepusha na huzuni kama hiyo.
Ninamtazama na maumivu aliyonayo na ninakubali kuwaza chaguo ambayo nimefanya Kupenda bila masharti na moyo ambao upo kwenye hatari lakini usio na hofu.
Kwa hivyo nikitazama nyuma ninaweza kusema sijutii kuhatarisha moyo wangu,
Ikiwa singependa kama nipendavyo, singekuwa na moyo ambao utavujika sana.
Kwa maana kama sikuwa nimempenda na kumpa yangu yote,
Singeweza kufikiria hisia ya kumpoteza kama simfahamu kabisa.

Lisa Twellman, 19/06/2005

Usikate Tamaa



hupaswi kamwe kukata
tamaa ya kuishi
wapo wengi wanaokuhitaji una mengi
sana ya kuwapa

Najua maisha yanaweza kuwa magumu
na kuna siku ambazo unazama wakati
mzigo ni mkubwa kiasi cha
kumshusha mtu yeyote

sasa mtazame Bwana
asimamaye kando yako na
uombe kwamba neno lake
itakua ndani yako

umepigana hapo awali na
ukakabiliana na hofu zako
za kuishi siku moja baada ya
nyingine
umezidisha miaka

kwa hivyo vaa silaha zako
na uchukue upanga wako
ili upigane na mawazo hasi
ambayo hatuwezi kumudu

Nitakuwa pamoja nawe kila
hatua ya safari hii
na kusherehekea ushindi
tunaposhinda kila siku

limeandikwa na baba: 20/06/2005



Kupitia Changamoto Maishani, Kuongozwa Na Lengo La Maisha

Unauliza ni nini maana ya maisha
Kwa nini tuko hapa duniani?
Kwa hasira tunapiga kelele na
mayowe
Kusudi letu haliko wazi sana

Wengine wanasema ni safari
Ni wakati tu ndio utabainisha
Wengine wanasema ni hatima
yetu Je, ni mbinguni au kuzimu

Mambo yanapoharibika maishani
Na mambo mabaya yanapotokea pande zote Je,
utakata tamaa kwa Kristo
Au utasimama kwenye Mwamba Imara?

Hakuna aliyeahidi kuwa itakuwa rahisi Kugeuza
shavu lingine
Kupuuza mabaya maishani
na kujitahidi kuwa mpole sana

Wivu na tamaa
Imejaa kwenye akili zetu za kimwili
Kutaka kile ambacho wengine wanacho
Ni sehemu ya mpango wa shetani

Kwa hivyo unapopitia changamoto za maisha
Na una wasiwasi kwamba ni jaribu
Shikilia imani yako milele
Wala usijali kuhusu mengine.

Limeandikwa na: baba: 23/06/2005

Kuelewa Saratani BILA Mungu

Mungu, kwa nini hili linatokea? Siwezi kusonga siwezi kupumua. Moyo wangu unauma, ninahisi kama unapindwa na kubanwa na kuvutwa pande kumi tofauti. Siwezi kuona. Machozi yanaendelea kufumba macho yangu. Ninajaribu kuyapepesa macho, Ninajaribu kujitia nguvu. Lakini ndani yangu ninaanguka, Mungu. Ndani yangu ninavunjika vipande vipande. Maisha yangu yanaangaza mbele yangu. Maswali yananizamisha. Mungu siwezi kufanya hivi. Sio kwa mara nyingine.

Maisha yangu yatakuwa vipi? Nywele zangu zimekua tu hivi maajuzi ilinichukua miaka mitatu. Tafadhali usiniondolee. Mipango yangu yatakuwaje? Ningependa kurudi San Diego. Ningependa kuenda shule kama watu wengine. Ninastahili kuhitimu miaka 3 ijayo. Nina azma ya kuwa mwalimu, maisha ya watoto ambao natakiwa kugusa yatakuwaje? Ni vipi kuhusu Familia yangu? Mama yangu. Baba yangu. Dada zangu. Ndugu yangu mdogo. Ninapaswa kuwa dada mkubwa mwenye nguvu. Siwezi kuwafanya wapitie hilo tena...ni afadhali nipitie peke yangu. Ningependa kuona Lisa na Laura wakifunga ndoa. Ningependa kusimamia harusi zao. Ningependa kumtazama Michael akihitimu kutoka shule ya upili. Ningependa kuwatunza Mama na Baba wanapozeeka. Sitaki iwe wao ndio wanaonitunza... haifai kuwa hivi.

Mungu bado ninazama...hali inazidi kuwa mbaya zaidi...niko kwenye ndoto mbaya.Haya si maisha yangu.Huu si mwili wangu. Ninaomba unipe mwili mpya kwa sababu huu umeharibika.Huu umenisaliti.

Mungu nimeshindwa kungoja.Kungoja huku kunaniumiza. Inanitafuna taratibu kwa njia isiyo nzuri. Mungu singependa kufanyiwa upasuaji, usiruhusu wanifanyie tena. Sitaki makovu mengine Bwana, watu watanipendaje nikiwa hivyo? Mungu usiwaache wanidhuru tena, wanifanye mgonjwa tena.Waambie waache kunipa IV, waambie waache kunidunga, waambie waache kuongea kuhusu kunifanyia kemotherapi tena. Baba, kwa sababu siwezi kufanyiwa tena. Sitaki kufanyiwa tena. Siwezi. Tafadhali usiwaruhusu kunitia sumu. Sitaki kutapika kila siku, Sitaki kuwa mgonjwa, Sitaki kutazama nyuso za wazazi wangu wanavyonisikia na kulazimika kuja mbio kuosha uchafu wangu. Sitaki kulala sakafuni tena nikiwa nimejikunja kwenye mpira. Ninapenda kitanda changu. Nayapenda maisha yangu sasa hivi. Tafadhali usiniondolee kila kitu. Si sasa.

Vipi kuhusu maisha yangu ya siku zijazo? Mungu, vipi kuhusu mwenzi wa roho yangu? Je, bado atanipenda nikiwa mgonjwa, bado ataniona mrembo wakati nitakapokuwa na upara na mweupe na nimedhoofika? Je, bado atataka kutazama macho yangu ya hudhurungi wakati yanamejaa giza na yamezama na kujaa machozi? Je, atakaa upande wangu? Je, atanikimbia? Vipi kuhusu familia ambayo ningependa kuwa na siku moja, Mungu? Vipi kuhusu watoto ambao ningependa kuwa nao? Hayley mdogo na Evan. Mungu, je, nitapata nafasi ya kuwatengenezea chakula cha mchana kila siku na kuandika "Nakupenda" kwenye nepi zao? Vipi kuhusu ujana wangu? Je, nitaweza kufurahia? Na kuishi kwa ukamilifu? Vipi kuhusu fukwe ambazo sijarambaza bado, milima ambayo sijapanda, marafiki ambao sijakutana nao, tabasamu ambazo sijatoa, maisha ambayo sijagusa bado Mungu? Bwana, kwa nini mimi? Mungu siwezi kufanya hivyo, ninahisi niko peke yangu, nahisi kukata tamaa, nahisi kuvunjika, nahisi kupotea. Nisaidie.

Kuugua Saratani UKIWA Na Mungu

Ee Bwana, wewe ni wa ajabu sana. Siwezi kusonga au kupumua kwa sababu nimevutiwa na upendo wako. Moyo wangu ulikuwa na uchungu na uliniokoa kutokana na hofu yangu. Moyo wangu umejaa pomoni na siwezi hata kujizuia jinsi ninavyohisi...Mungu amenijaza kila mahali, ninabubujikwa na furaha nyingi. Uwepo wako mzuri maishani mwangu unasisimua. Kwa njia nyingi, bado siwezi kuona Ee Bwana-kwa sababu karibu nimepofushwa na nuru yako! Mungu, nitaogopaje sasa? Nitawezaje kukuuliza maswali? Ninawezaje kukuhoji Wewe? Kwa mara moja ninasema ukweli kwamba siwezi kujiokoa kutokana na hili, ninazama. Lakini nikiwa na Wewe, kupitia Kwako, na kwa sababu Yako ninaweza kufanya mambo yote! Umechukua mzigo wangu, silazimiki kuubeba peke yangu ... haiwezekani. Lakini kwa kuwa ninajua tu kwamba Bwana wangu atakuwa mwaminifu daima ninapata tumaini ambalo singeweza kamwe kufikiria. Nimebarikiwa sana, lakini sistahili CHOCHOTE. Na nitakutumainia ewe Bwana, nitatumainia mpango wako kwangu, mapenzi yako kwangu, mpango wako kwa maisha yangu yajayo… na maisha ya sasa ambayo umenipa. Mungu, kwa nini mimi? Kwa nini umeyabariki maisha yangu kwa wingi na wema wako, upendo, na rehema? Mbona umejidhihirisha kwangu na kunipa nafasi Ya kupiga magoti yangu kwa ajili yako? Kwa nini umenibariki na uwezo wa kuona wakati kwa muda mrefu sana nilikuwa kipofu wa mpango wako wa ajabu na kusudi lako Takatifu? Kipofu wa utelewa maisha. Mungu, sitaacha kukusifu…wakati ninapopitia magumu, niwapo chini kabisa nitalisifu jina lako na kutabasamu kwa upendo wako wa ajabu kwangu. Siwezi hata kujizuia! Mimi ni mtu mpya. Kristo ameyabadilisha maisha yangu kwa njia ambayo sikuitarajia na ambayo sikuweza kuielewa. Mungu umejawa na neema! Upendo ulionibariki nao umejaa pomoni…neno ambalo ninalitumia mara kwa mara hivi sasa, lakini hakuna lingine linaloweza kuelezea maisha yangu vizuri zaidi! Moyo wangu umejawa na furaha na amani na upendo na kicho na ari ya kumtumikia Mungu. Nina furaha nyingi ndani yangu na ningependa kila mtu ajue na kuihisi, kwa sababu ni jambo la kushangaza na nzuri zaidi kuwahi kutokea na kila mtu anapaswa kuwa na fursa ya kulihisi. Mungu, ulimbadilishaje mtoto aliyevunjika, aliyechanganyikiwa, na aliyepotea kabisa kama mimi kuwa mfuasi mkamilifu na mnyenyekevu wa Yesu Kristo, aliye na moto kutoka ndani hadi nje na ujumbe Wako wa upendo na rehema? Sikujua hata nilikuwa kipofu. Sikuwahi hata kujua kuwa nilikuwa nikikosa mengi kwa muda mrefu. Sikujua kamwe nilikuwa na ganda la nje la ulinzi ambalo lilinilinda sana.Na sikuelewa kikamilifu jinsi ni vyema kufa kwa nafsi kwa ajili ya Kristo. Jinsi kufa ni kila kitu changu, kusalimisha kila kipande changu kunaweza kujaza moyo wangu na kunipa UZIMA kamili na usiopingika. Sitaogopa nikiwa na Kristo Yesu kando yangu, sitayumba-yumba katika upendo wangu na imani na kujitolea… haijalishi nitapoteza nini. Nimesema haya hapo awali na ninayaelewa hata zaidi sasa-unaweza kuchukua upendo wangu na afya yangu na maisha yangu, na sitaacha kamwe kumsifu Bwana Yesu Kristo. Hakuna kinachoweza kunyamazisha sifa kwenye midomo yangu kwa Baba yangu wa Mbinguni, hakuna kiasi cha uoga au giza au kutengwa au kuvunjika. Kwa kweli, nitamsifu hata zaidi. Ninaweka moyo na roho yangu yote katika Neno Lake na kusudi lake kwangu kwa sababu sina cha kupoteza na nina fursa ya kupata kila kitu.

Msifu Mungu Baba kwa kuwa ninaweza kutangaza wazi kwa uaminifu na kwa furaha kuwa,

"KUISHI ni Kristo, na KUFA ni faida."

Wafilipi 1:21

Mistari ya Bibilia Iliyopendwa na Familia

***Mama*:**
Bwana mwenyewe atakutangulia. Naye atakuwa pamoja nawe; kamwe hatakuacha wala hatakutupa. Usiogope wala usifadhaike. **Kumbukumbu la Torati 31:8**

***Baba*:**
Nasi tunajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hutenda kazi pamoja na wote wampendao, katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake. **Warumi 8:28**

***Laura*:**
Amebarikiwa mtu ambaye tumaini lake ni katika Bwana. Atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, uenezao mizizi yake karibu na kijito cha maji, na hauogopi wakati wa joto ujapo, majani yake ni mabichi daima, hauna hofu katika mwaka wa ukame na hautaacha kuzaa matunda. **Yeremia 17:7-8**

Kwa hiyo hatukati tamaa. Ingawa utu wetu wa nje unachakaa, utu wetu wa ndani unafanywa upya siku kwa siku. Kwa maana dhiki yetu nyepesi iliyo ya kitambo inatutayarisha kwa ajili ya utukufu wa milele unaozidi kuwa mwingi kupita kiasi. kwa sababu hatuangalii yale yanayoweza kuonekana, bali yale yasiyoweza kuonekana, kwa maana yale yanayoweza kuonekana ni ya muda tu, bali yale yasiyoweza kuonekana ni ya milele. **2 Wakorintho 4:16-18**

***Lisa*:**
Furahini pamoja na wenye kufurahi, lieni pamoja na wale waliao. Kaeni kwa amani ninyi kwa ninyi. Msijivune, bali mwe tayari kushirikiana na wanyonge. Wala msiwe watu wenye kujivuna kwamba mnajua kila kitu. **Warumi 12:15-16**

Zaidi ya yote, dumuni katika upendo kwa maana upendo husitiri wingi wa dhambi. Kuweni wakarimu kila mtu na mwenzake pasipo manung uniko. Kila mmoja na atumie kipawa chochote alichopewa kuwahudumia wengine, kama mawakili waaminifu wa neema mbalimbali za Mungu. **1 Petro 4:8-10**

***Michael*:**
Tunaishi kwa imani, si kwa kuona.
2 Wakorintho 5:7



Yesu Anapatikana Kwa Wote

Ilikuwa ni shauku ya Amanda na matamanio yake kabla ya kufa kwamba mashairi yake yachapishwe kwenye kitabu na kupewa wengine ili kuwaonyesha kuwa alipata nguvu zake kutokana na imani yake.

Alipoandika Kuelewa Saratani BILA Mungu na Kuugua Saratani UKIWA na Mungu, unaweza kuona kwa nini alichagua kuweka imani yake katika Yesu Kristo. Hakuzingatia tena ni pumzi ngapi angepumua, lakini mahali ambapo alikuwa anaenda baada ya pumzi yake ya mwisho.

Katika ukurasa unaofuata kuna mwaliko – kuwatia moyo wale ambao wamechochewa na safari ya Amanda katika imani. Nguvu ile ile iliyomtia nguvu Amanda na kusogeza mkono wake kuandika mashairi haya ya ajabu inaweza pia kukupa tumaini, kukutia moyo, na faraja. Ikiwa Amanda ameuchochea moyo wako kumjua Yesu na kupata nguvu na uwezo unaokuja na upendo unaopita fahamu, ninaomba uchukue wakati tulivu wa kutafakari na uyakabidhi maisha yako kwa Yeye pekee anayeweza kufanya zaidi ya yote tunayoomba au kufikiria.

Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

Yohana 03:16

Wakumbushe kwamba, "MIMI NIKO" anarudi tena
Tayarisheni njia, maana MFALME yuaja!

Ombi la Kuokoka

Ili uanze maisha yako mapya na Yesu kama Bwana na Mwokozi wako, hatua nzuri ya kwanza ni kuomba maombi yafuatayo, kutoka moyoni:

Baba yetu wa Mbinguni,
Ninajua kwamba nimekutenda dhambi na kwamba dhambi zangu zimenitenga na Wewe. Ninaomba Unisamehe. Ninajutia sana na sasa ningependa kugeuka kutoka kwa maisha yangu ya kale. Ninaamini kwamba Mwanao, Yesu Kristo, alikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zangu, kwamba alifufuka kutoka kwa wafu, yuko hai leo, na anasikia maombi yangu. Ninamwalika Yesu moyoni mwangu na kumwomba awe Bwana na Mwokozi wangu. Tafadhali tuma Roho Wako Mtakatifu anisaidie kukutii Wewe na kunisaidia kukufahamu na kufahamu upendo wako mkuu kwangu. Ninaomba unisaidie kuwa mtu ambaye Umenikusudia niwe. Nisaidie ili niweze kufuata mfano Wako na kufanya Mapenzi Yako maishani mwangu.
Ninaomba haya kupitia Jina la Thamani na Takatifu la Yesu Kristo aliye Bwana na Mwokozi wangu! Amina.

Ikiwa umeomba ombi hili, ni muhimu kuendeleza ukuaji wako wa kiroho na kuimarisha imani yako. Kama sehemu ya kuanzia, ninapendekeza kwamba uanze kwa kusoma Injili ya Marko au ya Yohana. Itakuwa vyema zaidi pia kujiunga na kanisa au kujiunga na kikundi kidogo cha kujifunza Biblia, ili kukuza uelewa wako. Ikiwa una maswali yoyote au ungependa tu kuzungumza na mtu, usisite kunipigia simu au kutuma barua pepe au ujumbe na nitafanya niwezavyo kukusaidia. Maelezo yangu ya mawasiliano yapo kwenye jalada la nyuma la Mashairi ya Amanda. Ukinipa jina lako nitakuombea.

Mpende Mungu - Wapende Wenzako

Mungu Mmoja Watu Wamoja



Katika kumbukumbu yenye upendo ya
Amanda Michelle (Twellman) Dieppa tarehe
10 Juni, 1982 - tarehe 19 Julai, 2005

Kwa vitabu vingine vya mashairi katika lugha ya Kiingereza,
Kihispania, Kichina, Kijapani, Kikorea, au Kiebrania tafadhali
tembelea tovuti ya www.amandaspoems.com
unaweza ama kumpigia simu Tom Twellman kwa (949) 923-1047
barua pepe: allmo108724@gmail.com

© Hakimiliki ya 2005, 2015, 2019, 2020, 2021, 2022, 2023